TANGAZO LA SERIKALI NA. 852 la tarehe 17/11/2023

SHERIA YA KANDA ZA UZALISHAJI KWA MAUZO YA NJE
(SURA YA 373)

# NOTISI

(*Imetengenezwa chini ya kifungu cha 3(1)*)

NOTISI YA TAMKO LA KANDA ZA UZALISHAJI KWA MAUZO YA NJE YA MWAKA 2023

Sura 373

KWA KUWA, Kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje, kinampa mamlaka Waziri, baada ya kushauriwa na Bodi na kwa kushirikiana na Mamlaka husika na kwa mapendekezo ya Mamlaka (EPZA), kupitia Notisi itakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali-

(a) kuanzisha au kutangaza eneo lolote la ardhi kuwa eneo la Ukanda wa Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje; na

(b) kuamua eneo, ukubwa na sifa halisi za mipaka ya eneo la Ukanda wa Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje.

NA KWA KUWA, Bodi ya Mamlaka ya Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje imemshauri Waziri kutangaza baadhi ya maeneo ya ardhi kuwa Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje na Waziri baada ya kushauriwa na kwa kushirikiana na mamlaka husika na mamlaka hizo kuridhia kutangazwa kwa maeneo ya ardhi yaliyowekwa kwenye Jedwali la Notisi hii;

Sura 373

HIVYO SASA, katika kutekeleza mamlaka niliyopewa

chini ya Kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Kanda za Uzalisha kwa Mauzo ya Nje, Mimi, KITILA ALEXANDER MKUMBO, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais- Mipango na Uwekezaji, natangaza maeneo yaliyoainishwa kwenye Jedwali la Notisi hii kuwa Kanda za Uzalisha kwa Mauzo ya Nje.

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Tamko la Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje ya Mwaka 2023.

Tamko la Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje

2. Maeneo ya ardhi yaliyoainishwa katika Jedwali la Notisi hii yametangazwa kuwa maeneo ya Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

MAENEO YALIYOTANGAZWA KUWA KANDA ZA UZALISHAJI KWA MAUZO YA NJE

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Eneo: | Eneo la Kinyanambo, Wilaya ya Mafinga, Mkowa wa Iringa. |
| | Kiwanja Na: | 4 - 6, Kitalu "S" |
| | Ukubwa wa Kiwanja: | 31,458 Mita za Mraba |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | Tractors Limited |
| | Jina la aliyepewa: | Ukanda wa Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje wa Briquette Energy Solutions. |
| 2. | Eneo: | Eneo la Msijute, Wilaya ya Mtwara, Mkoa wa Mtwara |
| | Kiwanja Na: | 121, 123 – 128, Kitalu "F" |
| | Ukubwa wa Kiwanja: | 7,144 Mita za Mraba |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | Jabiri Investment Limited |
| | Jina la aliyepewa: | Ukanda wa Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje wa Jabiri Investment. |
| 3. | Eneo: | Eneo la Kwemhosi, Kata ya Nkumba, Wilaya ya Muheza, Mkowa wa Tanga. |
| | Kiwanja Na: | 1, Kitalu "A" |
| | Ukubwa wa Kiwanja: | Ekari 1.16 |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | Jumuiya ya Wakulima wa Kilimo Hai Usambara Mashariki – (JUWAKIHUMA) |
| | Jina la aliyepewa: | Ukanda wa Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje wa N.T. Tanzania. |
| 4. | Eneo: | Eneo la Igomelo (Soko la Madini), Kata ya Maluga, Manispaa ya Kahama, Mkowa wa Shinyanga |
| | Kiwanja Na: | 189, Kitalu "D" |
| | Ukubwa wa Kiwanja: | 100 Mita za Mraba |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | Halmashauri ya Manispaa ya Kahama |
| | Jina la aliyepewa: | Ukanda wa Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje wa Stellar HMS. |

Dodoma,
3 Novemba, 2023

KITILA ALEXANDER MKUMBO
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-Mipango na Uwekezaji*